




Australian Government
Inspector-General of Taxation
Taxation Ombudsman

Una Malalamiko ya Ushuru?



Swahili

Sisi ni nani

Inspekta Mkuu na Mchunguzi Maalum wa Ushuru (The Inspector-General & Taxation Ombudsman (IGTO)) ni shirika huru la Serikali Kuu linalowajika kukusaidia na malalamiko yako kuhusu hatua za usimamizi za Ofisi ya Ushuru ya Australia (Australian Taxation Office (ATO)) na Halmashauri ya Weledi wa Ushuru (Tax Practitioners Board (TPB)).



1300 44 88 29 (Gharama
ya simu ya mahali ulipo)

Jinsi tunavyoweza kukusaidia

Tunatoa huduma huru, bila malipo, za ushuru za kitaalamu ili kukusaidia kushughulikia malalamiko yako.

‘Hatua za Usimamizi’ ni neno pana ambalo kwa jumla linashughulikia haki na mantiki ya matoleo au mawasiliano na wewe ya ATO au TPB.

Mifano ambayo IGTO inaweza kukusaidia, ni pamoja na lakini haijakomea kwa:

- wakati wa kufaa wa majibu ya maombi yako;
- tabia ya maafisa wa ATO au TPB;
- upatikanaji wa huduma za mtandaoni;
- hakikisho au utoshelevu wa ufafanuzi wa hatua za ATO au TPB;



- kuhakikisha hatua za ATO au TPB zinalingana na sera na taratibu zao; na
- kuhakikisha ATO au TPB inakutendea kwa njia ya haki na wazi na inazingatia maelezo yote ya husika yaliyotolewa, ikiwa ni pamoja na ukaguzi na uchunguzi.

Ikiwa huna uhakika kama tunaweza kukusaidia, tafadhali wasiliana nasi.

Ikiwa hatuwezi kukusaidia moja kwa moja, tutafanya kadri tuwezavyo ili kukupa ushauri kuhusu shirika au taasisi linalofaa zaidi kukusaidia.



GPO Box 551, Sydney NSW 2001

Mchakato wa malalamiko

Ili kuwasilisha malalamiko na ofisi yetu, angalia sehemu ya “Jinsi ya kuwasiliana nasi” (How to contact us).

Baada ya kuwasilisha malalamiko, afisa wa uchunguzi wa IGTU atawasiliana na wewe ndani ya siku 2 za kazi ili kutambua na kujadiliana na wewe kuhusu malalamiko yako.

Tutakusaidia moja kwa moja kushughulikia malalamiko yako ikiwezekana.

Huenda tukahitaji kupata maelezo yoyote ya ziada kutoka kwako, ATO au TPB ili kuelewa vyema malalamiko yako na kubainisha jinsi tunavyoweza kukusaidia vyema.

Tutakufahamisha kuhusu maendeleo yetu na kukupa muda wa uchunguzi wetu katika mchakato huu.

Jinsi ya kuwasiliana nasi



www.igt.gov.au



**1300 44 88 29 (Gharama ya
simu ya mahali ulipo)**



**GPO Box 551
Sydney NSW 2001**

Ikiwa unataka kuwasilisha malalamiko kwa lugha tofauti na Kiingereza piga simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS)), kwenye nambari ya simu **131 450**.

Ikiwa una ulemavu wa kusikia au kuongea na unaweza kufikia teletypewriter (TTY) au kifaa cha modemu, piga simu kwa **13 36 77**.

Ikiwa huwezi kupata TTY au kifaa cha modemu, piga simu kwa Huduma ya Kuwasilisha Mawasiliano, (Speech to Speech Relay Service) nambari ya simu **1300 555 727**.